

### Taarifa kwa Vyombo vya Habari

#### **serikali ya Bajwa-Imran Naipate Onyo kuwa Ummah Mtukufu wa Kiislamu Kamwe Hautakubali Kusalimisha Hata Shubiri Moja ya Ardhi Iliyo Barikiwa ya Palestina**

Huku Waislamu wa Pakistan wakiukataa kwa hasira mpango unaonadiwa na Amerika kati ya Imarati na umbile la Kiyahudi la kusawazisha mahusiano kikamilifu, serikali ya Bajwa-Imran kwa uangalifu inajitolea njia ya kukamilisha khiyana, pasi na kujali ima kukataa kata kata mpango huo wala hata kuushutumu. Siku hiyo hiyo Waislamu wa Pakistan walipoanzisha alama ishara ya Twitter **#UAESTabsMuslims**, mnamo 14 Agosti 2020, msemaji wa Afisi ya Kigeni ya Pakistan, Zahid Hafeez Chaudhri, alisema kwa tahadhari, "Ili kupatikana amani adilifu, pana na ya kudumu, Pakistan imeendelea kuunga mkono suluhisho la dola mbili kwa mujibu wa maazimio husika ya UN na OIC pamoja na kanuni ya kimataifa."

**Enyi Waislamu wa Pakistan!** Hakuna haki wala amani kwa Ummah wa Kiislamu ndani ya suluhisho la dola mbili. Umbile la Kiyahudi kwa ukamilifu wake ni uvamizi juu ya sehemu kubwa ya Ardhi Iliyo Barikiwa ya Palestina, ambalo ni lazima ling'olewe kwa ukamilifu wake. Uvamizi wa Ardhi za Kiislamu popote ulimwenguni, ima iwe na umbile la Kiyahudi upande wa Magharibi au Dola ya Kibaniani upande wa Mashariki, ni Fitnah ambayo ni lazima ipigwe vita, kwani Mwenyezi Mungu (swt), Mola wa Mashariki mbili na Magharibi mbili, ametuamrisha,

[وَأَقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُمْ مِّنْ حَيْثُ أَخْرَجْنَاكُمْ وَالْفِتْنَةُ أَشَدُّ مِنَ الْقَتْلِ]

**“Na wauweni popote mwakutapo, na muwatoe popote walipo kutoeni; kwani fitina ni mbaya zaidi kuliko kuuwa.”** [Surah al-Baqarah 2:191].

Ni kupingana na wale wanaozikalia Ardhi za Kiislamu, hadi uvamizi wao umalizwe, huku kuungana wa wale waliotufurusha kutoka katika ardhi zetu kumeharamishwa na Mwenyezi Mungu (swt),

[إِنَّمَا يَنْهَأُكُمْ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ قَاتَلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَأَخْرَجُوكُم مِّن دِيَارِكُمْ وَظَاهَرُوا عَلَىٰ إِخْرَاجِكُمْ أَن تَوَلَّوهُمْ ۗ وَمَن يَتَوَلَّهُمْ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ]

**“Hakika Mwenyezi Mungu anakukatazeni kufanya urafiki na wale walio kupigeni vita, na wakakutoeni makwenu, na wakasaidia katika kufukuzwa kwenu. Na wanao wafanya hao marafiki basi hao ndio madhaalimu.”** [Surah Al Mumtahina 60:9]. Ama dola dhaifu ya Palestina inayo pendekezwa katika suluhisho hilo la dola mbili, ni gereza la dhahiri, lilipewa kazi ya kuwazuia Waislamu ili walazimike kusalimu amri.

Maazimio ya UN na OIC yanakataliwa kwa sababu yanakiuka waziwazi maamrishi ya Mwenyezi Mungu (swt) na hivyo hayana thamani yoyote kwa Ummah wa Uislamu. Maazimio hayo ya Umoja wa Mataifa yameidhinishwa na wanachama wa kudumu wa Baraza lake la Usalama, dola za wakoloni ambao wao wenyewe wanazikalia Ardhi za Kiislamu na wamesaidia uvamizi wa umbile la Kiyahudi pamoja na Dola ya Kibaniani kwa zaidi ya miongo saba. Ama kuhusu maazimio ya OIC, yanatumiwa tu kuwazuia mamilioni ya vikosi vya majeshi ya Waislamu vya Ummah wa Kiislamu walio tayari na wenye uwezo, ili umbile la Kiyahudi pamoja na Dola ya Kibaniani ziweze kumakinisha mkono wao ndani ya Ardhi za Kiislamu pasi na changamoto yoyote.

Khiyana ya kihistoria dhidi ya Dini yetu tukufu inapanuka siku hizi, hivyo ni lazima isitishwe kabla haijafikia kilele chake, hivyo tufanyeni kazi ya kuiangamiza. Hakika, Ummah mtukufu wa Kiislamu umeamka kwa wajibu wake, na kuwakataa wale wanaoshirikiana na maadui, huku ukiwa na hamu ya dola ambayo itawalazimisha maadui wake kurudi nyuma. Ni juu yetu sote sasa kufanya kazi kwa umakinifu kwa ajili ya kuiregesha Khilafah kwa Njia ya Utume. Ni juu yetu sasa kuwasihi baba zetu, kaka zetu na watoto wetu walio ndani ya majeshi ya Pakistan kutoa Nusra yao kwa Hizb ut Tahrir, ili kuhukumu kwa yale yote yalioteremshwa na Mwenyezi Mungu (swt) kuanze, pasi na kuchelewa zaidi.

### **Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Pakistan**

Tovuti: [www.hizb-pakistan.com](http://www.hizb-pakistan.com) <http://HizbPK.page.tl>

Pepe: [HTmediaPAK@gmail.com](mailto:HTmediaPAK@gmail.com) WhatsApp: +90-531-814-7385

Twitter: <http://Twitter.com/HTmediaPAK>

Facebook: <https://Facebook.com/HTmediaPAK10>

YouTube: <http://YouTube.com/HTmediaPAK>

Dailymotion: <https://Dailymotion.com/HTmediaPAK>

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:

[www.hizb-ut-tahrir.org](http://www.hizb-ut-tahrir.org)

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:

[www.hizb-ut-tahrir.info](http://www.hizb-ut-tahrir.info)